

Siku moja katika mashindano fulani yaliyohusisha mabilioni ya washindanaji, yaliyokuwa na dhumiuni la kupata mshindi mmoja tu mwenye nguvu na mbio kuliko wengine.

Mashindano hayo yalikuwa na kanuni moja tu, inayosema ushinde uishi au ushindwe ufe. Hatimaye akapatikana mshindi mmoja tu ambaye hata leo hajitambui kuwa yeye aliwahi kushinda mashindano hayo hata kabla hajavuta pumzi ya dunia.

Unazani huyo mtu ni nani? Ni wewe unayesoma maneno haya sasa. Tangu ukiwa tumboni mwa mama yako ulikuwa mshindi na hata sasa wewe ni mshindi, lakini hulitambui hilo.

Ulipozaliwa ulianza kujifunza vitu ulivyovikuta wakiwa navyo wazazi au walezi wako, ulijifunza mifumo yao ya maisha, imani, utamaduni n.k na ndivyo vitu haswa vilivyojenga fikra zako. Baada ya wazazi kukulea kwa muda fulani walikupeleka shuleni kwa mtazamo kwamba utaenda kupata vitu bora zaidi kuliko walivyokuwa navyo wao, utajifunza vitu bora zaidi kuliko walivyo kufundisha wao.

Lakini kitu cha hatari zaidi ni kuwa ulipokwenda shuleni ulikwenda kupambana na mitihani badala ya ujinga.

Shuleni pamekuwa mahali pa kutengeneza watu tegemezi na wenye uwezo mdogo wa kufikiri badala ya kutengeneza watu watakao kuwa msaada kwa jamii. Leo bila vyeti

wengine hawawezi kufanya chochote. Huo ni ugonjwa wa ufikiri.

Kama watu ni wagonjwa wa fikra basi hawawezi kufikiri kuboresha maisha yao kwa uwezo wao ila watahitaji kuiga na kupata msaada kutoka kwa wale wanaojua kufikiri.

Tumekuwa watumwa katika nchi ambayo tunasema ni nchi huru, hivyo hatuutendei haki ule uhuru wa nje tulio upata kwa sababu bado ndani yetu tuwafungwa.

Chanzo cha maendeleo yejote ni fikra, uwezo wa kufikiri zaidi ya matatizo tuliyo nayo ili kuyatafutia utatuvi. Sasa wengi wetu tunakimbia matatizo badala ya kuyatatuvi. Hii ni ishara tosha kuwa tunaufikiri finyu. Huu ndio ugonjwa unaotusumbua wengi, unaitwa utumwa wa fikra.

Tuna rasiliamali nyingi katika mazingira tuliyo nayo kuliko tunavyozani, lakini kutokana na ufinyu wa ufikiri na mzigo wa utumwa tulio nao kwenye akili zetu tunashindwa kuzitumia kutengeneza maisha yetu kuwa bora. Hatuwezi kuziona fursa kwasababu macho ya fursa yanapatikana kwenye fikra za mtu.

Jambo la muhimu kujua ni kuwa huwezi kuishi maisha yako halisi yaliyojaa mafanikio kama umekuwa mtumwa wa fikra. Utumwa wa fikra huleta uvivu wa kufikiri unaopelekea kutokuwa wabunifu au uzalishaji finyu unaosababisha kutowajibika.

fikra ndio ikulu ya mafanikio, hakuna mafanikio ambayo hayakuanza na wazo. Hivyo ukitaka kuzuia mafanikio na maendeleo zuia watu wasifikiri.

Nina habari njema kukukaribisha ujifunze pamoja nami namna ya kutoka katika gereza hili gumu na kuishi maisha yako halisi yaliyojaa mafanikio ya kila aina.